

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

KUMB. NA MDC/DED/L5/50/VOL. III/32

23/09/2019

KWA WADAU WOTE WA UCHAGUZI

MAELEKEZO YA UCHAGUZI

Maelekezo kuhusu Uchaguzi ni kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (1) na (2) (a) hadi (k)

1. Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya uchaguzi siku sitini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.
2. Maelekezo ya Uchaguzi, kwa mujibu wa Kanuni hizi, ni kama ifuatayo:-
 - a) Tarehe ya kufanyika kwa uchaguzi itakuwa tarehe 24/11/2019
 - b) Muda wa kufanyika uchaguzi utakuwa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni,
na mahali pa kufanya uchaguzi ni katika kila Kitongoji mahali palipoainishwa.
 - c) Muda wa kuandikishwa Wapiga Kura utakuwa ni kuanzia tarehe 8 – 14 Oktoba 2019 saa 2:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni,
na sehemu ya kuandikishwa Wapiga Kura ni katika kila kitongoji mahali palipoainishwa.
 - d) Wakazi wote wenye sifa za kupiga kura wanatakiwa kushiriki uchaguzi huu ni haki yao.
 - e) Wakazi wenye umri wa miaka ishirini na moja au zaidi wanaotaka kugombea nafasi ya Uenyekiti wa Kijiji au Uenyekiti wa Kitongoji au Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji (Wajumbe mchanganyiko na Wanawake) wachukue fomu za kugombea zitakazopatikana kwenye Ofisi ya Msimamizi Msidizi wa Uchaguzi kwa utaratibu uliopangwa.
 - f) Muda wa kuchukua fomu ni tarehe 29 Oktoba 2019 na kurudisha fomu za maombi ya kugombea uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji kwa msimamizi wa Uchaguzi ni tarehe 29 Oktoba hadi 4 Novemba 2019.
 - g) Siku ambayo uteuzi utafanyika ni tarehe 5 Novemba 2019 na sehemu ya matangazo ya uchaguzi ambapo fomu za wagombea zitabandikwa ni katika Ofisi za Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi.
 - h) Muda wa kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi ni tarehe 5 Novemba hadi 6 Novemba 2019 na kusikilizwa kwa pingamizi.
 - i) Tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi uamuzi wa Msimamizi Msidizi wa Uchaguzi ni tarehe 5 Novemba hadi 9 Novemba 2019.
 - j) Kipindi cha kuendesha mikutano ya Kampeni za Uchaguzi ni siku saba kuanzia tarehe 17 Novemba hadi 23 Novemba 2019.
 - k) Masuala mengine yanayohusu uchaguzi yanapatikana kwenye Kanuni na Mwongozo wa Uchaguzi wa 2019

Maelekezo yametolewa na


HORACE KOLIMBA
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA WILAYA
MBULU


HORACE KOLIMBA
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA WILAYA
MBULU